

النبي القدوة (صلى الله عليه وسلم) في بيته وحياته

" Mtume ambaye ni Ruwaza njema (S.A.W) katika nyumba na maisha yake"

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote, anayesema katika Qur'ani Tukufu:

"لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ"

"Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.", na ninashuhudia kwamba hakuna Mungu ila Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kwamba Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni mja na Mtume wake, Ewe Mwenyezi Mungu sala na salamu zimwendee yeye na familia yake na Maswahaba wake na kila atakayewafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

Amma baada ya utangulizi huu

١- Ndugu zangu Waislamu, hakika Mwenyezi Mungu (S.W) alimchagua na alimteua Mtume Wake (S.A.W) juu ya viumbe vyote, na akamkunjulia kifua, akamwinua daraja, akaunyanyua utajo wake, na akampa sifa zote kamilifu za mwanadamu, kwa hivyo Mtume (S.A.W) alikuwa mtu mkamilifu zaidi kwa tabia njema, mwenye roho nzuri zaidi, ana moyo safi kabisa, alikuwa na akili nzuri zaidi, na mbora wao katika kutangamana na watu, ambapo Mwenyezi Mungu (S.W) anasema:

" وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ "

"Na hakika wewe una tabia tukufu".

2- Na yule anayetafakari katika maisha ya Mtume wetu (S.A.W) ataona kwamba yeye alikuwa ndiye ruwaza njema kwa wanadamu wote, ambapo Mwenyezi Mungu (S.W) anasema:

"لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِمَن كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ

كَثِيرًا"

"Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana"
Kwa hivyo Mtume (S.A.W) ndio mume bora zaidi, ndio baba mzuri, na ndio babu mzuri, haswa kwa kuwa yeye (S.A.W) alisema:

"خَيْرُكُمْ خَيْرُكُمْ لِأَهْلِهِ، وَأَنَا خَيْرُكُمْ لِأَهْلِي"

"Mbora wenu ni aliye mbora kwa familia yake, na mimi ndiye mbora wenu kwa familia yangu"

3- Ni nzuri sana kutazama kwa tabia zake (S.A.W) katika nyumba yake, na jinsi anavyotendea familia yake, ambapo mkewe Khadija (R.A), akimsifu (S.A.W) akisema:

"كَلَّا لَا يَخْزِيكَ اللَّهُ أَبَدًا إِنَّكَ لَتَنصِلُ الرَّحِيمَ، وَتَحْمِلُ الْكَلَّ، وَتَكْسِبُ الْمَعْدُومَ، وَتَقْرِي

الصَّيْفَ، وَتُعِينُ عَلَى نَوَائِبِ الْحَقِّ"

"hapana, Mwenyezi Mungu hatakuhizi kamwe, kwani wewe unawasiliana na jamaa zako, unawasaidi wahitaji, unwapa maskini, unamkarimu mgeni, na unamsaidia aliyepatwa na msiba" Mtume (S.A.W) alikuwa anahifadhi agano lake baada ya kifo chake; mfano wa hayo ni kwamba mwanamke mzee alikuwa anamtembelea Mtume (S.A.W) na Mtume alikuwa anasimam kwake na anamheshimu, wakati hii

bibi Aisha alimuuliza Mtume (S.A.W) kuhusu siri ya kumheshimu, akasema: (S.A.W)

"إِنَّهَا كَانَتْ تَأْتِينَا عَلَى عَهْدِ خَدِيجَةَ، وَإِنَّ حُسْنَ الْعَهْدِ مِنَ الْإِيمَانِ"

"hakika yeye alikuwa anatukujia wakati wa Khadija, na agano zuri ni kutoka imani" na alikuwa anasema: (S.A.W) juu ya mama wa waumini Khadija: (R.A)

"مَا أَبَدَنِي اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ خَيْرًا مِنْهَا، قَدْ آمَنَتْ بِي إِذْ كَفَرَ بِي النَّاسُ، وَصَدَّقَنِي إِذْ كَذَّبَنِي النَّاسُ، وَوَأَسْتَنِي بِمَالِهَا إِذْ حَرَمَنِي النَّاسُ، وَرَزَقَنِي اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ وَلَدَهَا"

"Mwenyezi Mungu (S.W) hakunipi mke mzuri badala yake, kwani yeye akaniamini wakati watu walinikufuru, akanisadiki wakati watu wakanikadhibisha, akanifariji kwa mali yake wakati watu walinizua mali yao, na Mwenyezi Mungu aliniruzuku mtoto kutoka kwake"

ξ- Pia, Mtume (S.A.W) alikuwa anaisaidia familia yake katika mahitaji yao, ambapo bibi Aisha (R.A) anasema: "Yeye (S.A.W) alikuwa anashona nguo zake, anashona viatu vyake, na alikuwa anafanya wanachofanya wanaume nyumbani yao, bibi Aisha (R.A) aliulizwa: "Je!, Mtume (S.A.W) alikuwa anafanya nini nyumbani yake? alisema: alikuwa anafanya kinachokifanya familia yake, na wakati wa sala ulipofika, alikuwa anatawadha na anakwenda ili kusali. Bali, Mtume wetu (S.A.W) alikuwa na hamu ya kuwafurahisha watu wa nyumba yake, kwa kutenga muda kwa ajili ya kukaa pamoja nao, mfano wa hayo, wakati wa kuingia usiku alikuwa (S.A.W) anatembea na bibi Aisha (R.A) na wakati mwingine huzungumza naye.

ο- Na binti zake (S.A.W) walikuwa na sehemu kubwa ya fadhili na ukarimu wake, binti yake Fatima (R.A), alipokuwa akiingia juu yake (S.A.W), alikuwa anamsimamia, akamshika mkono, akambusu, na akamketisha mahalini pake, na (S.A.W) alipokuwa akiingia juu ya binti yake, alikuwa anamsimamia,

akamshika mkono, akambusu, na akamketisha mahalini pake, ambapo bibi Aisha (R.A) anasema:

"Wake wa Mtume (S.A.W), walikuwa pamoja naye, Fatima (R.A) alikuja akitembea, akienda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.A.W), alipomwona, alimkaribisha na akasema "Karibu, binti yangu", kisha akamketisha karibu naye (S.A.W)".

Ninasisema kauli yangu hii na ninamwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu msamaha kwa ajili yangu na yenu.

الحمد لله رب العالمين والصلاة والسلام على أشرف المرسلين سيدنا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين، ثم أما بعد،،،

Ndugu zangu waislamu tunazungumza katika hotuba yetu ya pili juu ya "tabia ya Mtume (S.A.W) pamoja na watu wa nyumba yake"

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola Mlezi wa viumbe vyote. Na ninashuhudia kwamba hakuna Mungu mwingine yeyote anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, yeye pekee asiye na mshirika wake. Na ninashuhudia kwamba Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni Mja na Mtume wake. Ewe Mola Wetu Mlezi tunakuomba umswalie, umrehemu na umbariki yeye na jamaa zake na Maswahaba wake wote na kila atakayewafuata mpaka siku ya Malipo.

Ndugu zangu Waislamu:

1- Mtume wetu (S.A.W) alikuwa babu bora kwa wajukuu zake, akiwaheshimu, akiwahurumia, na alikuwa mwema pamoja nao, mfano wa hayo ni kwamba yeye (S.A.W) alikuwa anatoa hotuba, akawaona mabwana wawili, Hassan na al-Hussain (R.A) wakimjia, wakiwa wamevaa mashati mekundu, walikuwa wanaanguka kisha wanasimama tena, basi Mtume (S.A.W) aliwashukia, akawakumbatia, na akawachukua naye juu ya mimbari. Na wakati mwingine Mtume (S.A.W) akamwona Bwana wetu al-Hussain (R.A) anacheza na wavulana wawili barabarani, basi yeye (S.A.W) akanyosha mikono yake, na al-Hussain akaanza (R.A) kukimbilia hapa na pale, na Mtume (S.A.W) anamcheka yeye mpaka akamchukua, akambusu, na akasema:

"حُسَيْنٌ مَّيِّ، وَأَنَا مِنْ حُسَيْنٍ، أَحَبُّ اللَّهِ مِنْ أَحَبِّ حُسَيْنًا"

"Hussain ni wa mimi, na mimi ni wa Hussain, Mwenyezi Mungu anampenda kila anayempenda Hussain"

2- Siku moja, Mtume (S.A.W) alikuwa akisali kwa watu, mjukuu wake bibi Umamah (R.A) alimjia, basi alikuwa (S.A.W) anambeba mikononi mwake wakati alipokuwa anasimama, na alikuwa anamweka chini wakati alipokuwa anasujudu. Pia, Mtume (S.A.W) alikuwa anamcheza Zainab, binti ya mkewe bibi Umm Salamah (R.A), akisema: **"Ewe Zainabu, Ewe Zuwainabu, mara kwa mara"**

3- Kwa hivyo, Ndugu zangu Waislamu, tunahitaji kumfuata Mtume wetu (S.A.W) katika mambo yote ya maisha yake, kwani yeye (S.A.W) alikuwa mwingi wa rehema kwa watu, mkarimu zaidi, msemaye kweli zaidi, mwadilifu zaidi, na shujaa zaidi, bila shaka kumwiga na kumfuata ni moja ya dalili ya upendo wake (S.A.W), ambapo Mwenyezi Mungu (S.W) anasema:

"قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ"

"Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuatani mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu."

Ewe Mwenyezi Mungu, utupe uwezo wa kumfuata vizuri Mtume wako (S.A.W), na utupe ufahamu katika dini yetu, uilinde nchi yetu, na nchi zingine za Walimwengu wote.

والسلام عليكم ورحمة الله وبركاته